



**Tanzania
Media Fund**

TMF is managed by Hivos Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Waandishi wa Habari Wapata Changamoto Kuongeza Ubora wa Taarifa Wanazoandika

Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), mfuko mpya utakaoendeshwa kwa miaka mitatu kuimarisha uandishi wa habari za uchunguzi na uandishi wa habari unaozingatia ubora, utazinduliwa rasmi siku ya Jumatano tarehe 3 Desemba 2008 katika ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam kuanzia saa 10.30 alisiri hadi saa 1.00 jioni.

Uzinduzi huo wa aina yake utahusisha hotuba ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, filamu na mdahalo wa wazi.

Spika, Mheshimiwa Samwel Sitta, anatarajiwa kuwapa changamoto washiriki kuhusu wajibu wa vyombo vya habari katika kukuza uwajibikaji wa umma na utawala, na kujadili uhuru wa vyombo vya habari pamoja na mahusiano ya bunge na vyombo vya habari.

Wazungumzaji maarufu: Ayub Rioba, Kajubi Mukajanga, Salva Rweyemamu, Sakina Dato na Vicky Ntetema watajadili mada kuhusu: Je serikali ndicho kikwazo kikuu dhidi ya uandishi wa habari unaozingatia ubora? Ni vyombo vya habari vyenyewe? Au tatizo ni jamii iliyolala? Jenerali Ulimwengu ataongoza mdahalo huo.

Uzinduzi huo utanza kwa filamu fupi ikiwaonyesha wananchi wakitoa maoni yao kuhusu vyombo vya habari Tanzania.

Hafla itatanguliwa na mkutano wa kuwapa taarifa waandishi wa habari na watu wengine wanaotarajiwa kuomba ruzuku kutoka TMF utakaoanza saa 9.00 alisiri hadi saa 10.30 alisiri.

TMF imeanzishwa hivi karibuni ili kusaidia katika kuboresha taaluma ya uandishi wa habari Tanzania kwa kuwapatia waandishi wa habari pamoja na mashirika yanayojishughulisha na kazi za kihabari (Machapisho, luninga na redio):

- Huduma ya fedha za ruzuku, na
- huduma ya mafunzo yatakayotolewa kwa njia ya mafunzo kazini, kuzoeza, nasaha na kwa njia ya mtandao kwa wale watakaopatiwa ruzuku

Dira ya TMF ni kuiona jamii wazi ikitoa na kupata habari na kujadili fikra tofauti kwa uhuru. TMF inadhamiria kuendeleza uwezo wa vyombo huru vya habari, vinavyomilikiwa na watu tofauti na vyenye nguvu kwa kuwezesha uandishi wa habari za uchunguzi na za matakwa ya umma zenye kuzingatia uchambuzi wa kina na zenye manufaa kwa watu wa kawaida.

Mtazamo wa TMF kuhusu habari za uchunguzi ni uandishi wa kubainisha ukweli uliojificha ambao usingefahamika bila ya kufanya utafiti wa kina. Inajumuisha utafutaji wa taarifa kwa umakini, kuthibitisha taarifa kupitia vyanzo tofauti, uchambuzi na kuandika vizuri. Uandishi wa habari zenye matakwa ya umma unajumuisha ubora na utafiti wa kina kuhusu jambo lenye umuhimu mkubwa au linalowahusu watu wa kawaida, hasa wale ambao ni masikini na wanyonge.

TMF inatambua kwamba uandishi wa habari za uchunguzi na zile za matakwa ya umma unawalazimu waandishi wa habari kuzingatia ubora na usawa, kitu ambacho kinahitaji umakini na jitihada za hali ya juu.

Mfuko wa vyombo vya habari Tanzania umedhaminiwa kwa pamoja na Shirika la Maendeleo la Uswisi (Swiss Development Cooperation (SDC), Ubalozi wa Denmark (Danish Embassy), Ubalozi wa Ufalme wa Uholanzi (Embassy of the Kingdom of the Netherlands), Serikali ya Ireland (Irish Aid) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Serikali ya Uingereza (Department for International Development (DfID)). Jumla ya fedha kwa ajili ya kipindi cha miaka mitatu ni Dola za Marekani milioni saba nukta moja (USD. 7.1. million) ambayo ni takriban shilingi bilioni nane na nusu za Tanzania (TZS. 8.5 billion shillings).

Imesainiwa na:

Marjan Besuijen
Meneja Mkuu

(Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na Ernest Sungura, Meneja anayeshughulikia Ruzuku, kupitia namba ya simu 0754 760068)

Tanzania Media Fund
1124 Barabara ya Chole , Masaki, S.L.P. 38266, Dar Es Salaam, Simu +255-22 2601080/2,
Faksi: +255-22 2601096, Barua pepe: info@tmf.or.tz